

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

**Simu:** 255-262961500/1  
**Nukushi:** 255-262961502  
**Baruapepe :**  
press@ikulu.go.tz  
**Tovuti :** [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



**OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS  
NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.**

**Dar es Salaam**  
**30 Septemba, 2023**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**RAIS SAMIA AZINDUA TOVUTI YA NYARAKA ZA DKT. SALIM AHMED SALIM**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amekibadilisha jina Chuo cha Diplomasia nchini na kukipa jina la Waziri Mkuu Mstaafu Dkt. Salim Ahmed Salim.

*“Na kwasababu mcheza kwao hutunzwa, na tumesema alikuwa mwanadiplomasia mahiri, tumekubaliana kukipa Chuo kile cha Diplomasia jina na sasa rasmi kitakuwa kinaitwa Dr. Salim Ahmed Salim Centre for Foreign Relations.”*

Aidha, Rais Samia amesema lengo la kukipa jina hilo ni kuonesha mchango uliotolewa na mwanadiplomasia Dkt. Salim ambae alifanya kazi kwa muda mrefu katika nyanja ya kidiplomasia ya kimataifa kwa nidhamu bila kukata tamaa.

Rais Samia amesema hayo leo kwenye hafla ya uzinduzi wa tovuti ya nyaraka za Dkt. Salim Ahmed Salim, iliyofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere.

Rais Samia amemuelezea Dkt. Salim kama kiongozi aliyethamini elimu katika jamii na aliyesaidia watu wengi kufikia maendeleo na ndoto zao kwa kutoa ushauri na mafundisho mbalimbali.

Rais Samia ameeleza kuwa katika uongozi wake, Dkt. Salim alitoa mchango mkubwa katika uhamasishaji wa masuala ya uzalendo, muungano na umaja ambao yalichangia katika kudumisha amani na umaja wa taifa.

Rais Samia ametoa wito kwa viongozi wa umma kuiga mfano wa Dkt. Salim kwa kutunza kumbukumbu za maisha yao kwa manufaa ya vizazi vya sasa na baadae ili zisaidie kukuza na kuimarisha uelewa wa juhudhi za kila kiongozi, historia ya nchi na bara la Afrika.

Zuhura Yunus  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

